JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

MFUKO WA PEMBEJEO (AGITF)

Kwa Mawasiliano:-

Mkurugenzi Mtendaji
Mfuko wa Pembejeo
S.L.P 2382 DODOMA
Simu 0262354166
Nukushi/fax 0262350268
Barua Pepe info @agitf.go.tz Tovuti www.agitf.go.tz

ITANGULIZI

Mfuko wa Pembejeo ni Taasisi ya Serikali inayotoa mikopo ya pembejeo za Kilimo, Mifugo na Uvuvi pamoja na zana za kilimo. Mikopo inayotolewa na Mfuko wa Pembejeo ni kwa ajili ya kupanua maeneo ya kilimo na kuongeza uzalishaji katika sekta ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi. Muda wa mkopo ni kati ya miaka miwili (2) hadi mitano (5), kutegemea aina ya mkopo. Riba ya mkopo ni asilimia sita (6%) hadi nane (8%).

DIRA

Kuwa kinara chaguo katika kutoa mikopo ya pembejeo na zana kwa riba nafuu kwa wakulima/wafugaji na wavuvi wadogo katika kuitikia wito wa mahitaji ya maendeleo ya kilimo Tanzania.

DHIMA

Kutoa mikopo ya riba nafuu kwa wakulima, wafugaji na wavuvi wadogo nchini Tanzania ili kuboresha maisha ya kaya pamoja na usalama wa chakula wa Taifa.

MADHUMUNI

Kupanua maeneo ya kilimo na kuongeza uzalishaji katika sekta ya kilimo, mifugo na uvuvi

WALENGWA WA MFUKO.

Walengwa ni wakulima binafsi , makampuni, vikundi na Taasisi za kijamii zililizosajiliwa na zinazojishugulisha na kilimo; wasambazaji wa pembejeo za kilimo, mifugo na uvuvi, pamoja na wenye viwanda vya kuongeza thamani ya mazao ya kilimo na mifugo.

5. AINA ZA MIKOPO NA TARATIBU ZAKE

i. Pembejeo za kilimo, Mifugo na uvuvi

- Mwombaji / kikundi kitajaza fomu ya maombi ya mkopo ambapo fomu iliyokamilishwa itaidhinishwa na Halmashauri husika anakofanyia shughuli inayoombewa mkopo.
- Muda wa mkopo ni miaka 2 na riba ni 8% kwa mtu binafsi na 6% kwa vikundi.

ii. Matrekta ya mikono (powerTiler)

Muda wa mkopo ni miaka 3 ikijumuisha na muda wa rehema , (grace period). Riba ni 6% kwa vikundi na 7% kwa mtu binafsi.

iii. Mitambo ya mashambani (farm machinery)

Mkopo huu ni matrekta mapya, zana za kuvunia, kupandia, magari ya kubeba mazao, mashine za kukamulia maziwa, kupakia miwa, kufyeka na kufungia nyasi, kutengeneza chakula cha mifugo, nk

Mkopaji atatakiwa kuchangia ununuzi wa mtambo husika kwa asilimia (10%).

Muda wa mkopo ni miaka 5 ikijumuisha na muda wa rehema, (grace period) na riba ni 7% kwa mtu binafsi na 6% kwa vikundi

iv. Ukarabati wa matrekta

Muda wa mkopo ni miaka 2 ikijumuisha na muda wa rehema (grace period). Riba ni 6% kwa vikundi na 7% kwa mtu binafsi.

v. Mikopo ya miundombinu ya kilimo mifugo na uvuvi

- Hii ni pamoja na maghala, shamba kitalu 'green house', nyumba ya shambani, mabanda ya kuku/ nguruwe/ ng'ombe, mizinga ya nyuki, visima, mabwawa, vifungo vya kutibia na kuogeshea mifugo, mashimo ya kutunza vyakula vya mifugo nk.
- Muda wa mkopo ni miaka 3 na miezi 6 ikijumuisha na muda wa rehema wa miezi 6, na riba ni 7% kwa mtu binafsi na 6% kwa vikundi.

vi. Mikopo ya fedha za kuendeshea shughuli za shamba (farm operations)

- Muda wa mkopo ni miaka 2 na miezi 6 ikijumuisha na miezi 6 ya muda wa rehema. Riba ni 7% kwa mtu binafsi na 6% kwa vikundi
- Mwombaji awe na ardhi ya kufanyia kazi au awe na mkataba wa kukodi ardhi hiyo kwa muda wa miaka 3 au zaidi.

vii). Mikopo ya kununua ardhi kwa ajili ya kilimo, ufugaji au uvuvi.

- Muda wa mkopo ni miaka 4 ikijumuisha na muda wa rehema, wa miezi 12; na riba ni 7% kwa mtu binafsi na 6% kwa vikundi
- Ardhi iwe inamilikiwa kisheria na mkopaji awe na uzoefu wa kutosha katika shughuli anayokusudia kuifanya.

viii). **Zana unganishi (farm implements;)-**

- Hizi ni "*trailers, harrows, disc ploughs, bonesaw, carcass saw, spitting, ban, water pump, storage and cold chain equipments chiller, insulated container, meat van, deepfrezers, refrigerators, liguid nitrogen containers, coolboxes and cans)*"
- Muda wa mkopo ni miaka 3 ikijumuisha na muda wa rehema, (grace period) ya miezi 6; na riba ni 7% kwa mtu binafsi na 6% kwa vikundi

ix). **Mikopo ya zana za kusindika na vifungashio vya mazao ya kilimo, mifugo na uvuvi**

Muda wa mkopo ni miaka 3 ikijumuisha na muda wa rehema, (grace period) ya miezi 6; na riba ni 7% kwa mtu binafsi na 6% kwa vikundi

x) **Mikopo kwa taasisi kwa ajili ya kukopesha (on lending/wholesale).**

- Riba ya mkopo ni asilimia (4%), na Taasisi/Asasi husika itamkopesha mkulima kwa riba ya 6% kwa mwaka.
- Muda wa mkopo ni miaka 3 ikijumuisha na muda wa rehema (grace period) ya miezi 6.

6. DHAMANA ZA MIKOPO

6.1 Mtu binafsi / Makampuni / Asasi zenye mali isiyohamishika.

Dhamana ya mkopo ni nyumba, shamba, au kiwanja chenye hati miliki.

6.2 **Vikundi/SACCOS/AMCOS**

Dhamana ya mkopo kwa vikundi na vyama vya ushirika visivyo na hati miliki ni asilimia 30% ya mkopo wanaoomba kutoka kwenye akiba zao na 70% ya mkopo itadhaminiwa na Halmashauri (kikao cha kamati ya fedha na mipango).

6.3 **Watumishi walio na mikataba ya kudumu**

Dhamana za mishahara kwa waombaji walio kwenye ajira rasmi wenye mikataba ya kudumu na mishahara yao inakidhi makato kwa muda wote wa mkopo. Marejesho ya mkopo yatafanywa na mwajiri kila mwezi kutoka katika mshahara wa mkopaji na kuwasilishwa kwenye account za Mfuko moja kwa moja.

6.4 **Benki Jamii/Community Bank**

Dhamana ya mikopo kwa Benki Jamii ambazo hazina hati miliki ni pamoja na nyaraka zinazoonyesha usajili, pamoja na kiwango cha chini cha mtaji (minimum core capital) kama inavyoelekezwa na Benk Kuu.

RAS-